MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA BIMA NCHINI (TIRA)

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAMLAKA KUFUTA LESENI KWA BAADHI YA MAKAMPUNI YA UDALALI WA BIMA NCHINI MWAKA 2018.

Ndugu waandishi wa Habari.

Leo tarehe **22.03.2018** Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Nchini (TIRA) kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na.10 ya mwaka 2009 inayoipa Mamlaka ya kuishauri serikali kuhusu masuala na mwenendo wa soko la bima nchini imewaita hapa ili kuwaelezea na kuwapa taarifa umma wa watanzania kuhusu kufuta leseni kwa makampuni **manne 4** ya ushauri na udalali wa bima (Insurance Brokers).

Ifahamike kuwa, makampuni ya udalali na ushauri wa Bima (Insurance Brokers) ni makampuni yaliyosajiliwa na kupewa leseni ya kufanya biashara ya bima kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na.10 ya mwaka 2009.

Makampuni haya ya udalali na ushauri yana wajibu wa kumshauri mteja au mkata bima kukata bima sahihi kulingana na aina ya janga au vihatarishi vinavyoweza kumpata. Pia, yanawajibika

kumwakilisha mteja wa Bima kwa kampuni ya Bima ikiwa mteja atapata janga linalohitaji fidia.

Pia, makampuni haya huwajibika kwa makampuni ya bima (Insurance Companies) kwa kutafuta wateja wa bima na kuuza aina mbalimbali za bima za makampuni yaliyosajiliwa na kupewa leseni na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima.

Katika shughuli za usimamizi wa soko la bima nchini, Mamlaka imebaini ukiukwaji wa sheria ya Bima Na.10 ya mwaka 2009 inayotoa taratibu za ufanyaji biashara ya bima nchini kwa baadhi ya makampuni ya udalali wa bima.

Ndugu waandishi wa Habari.

Kutokana na malalamiko yanayopokelewa na Mamlaka imeonekana baadhi ya makampuni ya udalali wa bima yamekuwa yakikiuka taratibu za uendeshaji biashara za bima hivyo kuchafua taswira ya biashara ya bima na kutishia uhai wa soko la bima nchini. Makampuni haya yameshindwa kuwasilisha tozo za bima kwa makampuni ya bima hivyo kuwanyima wateja wa bima haki ya kunufaika na fidia ambazo zingetolewa na makampuni ya bima endapo fedha hizi zingewasilishwa. Makampuni yaliyofutiwa leseni ya udalali wa bima ni kama yafuatayo;

i. **Kampuni ya Udalali wa Bima ya HANS**

Moja wa wateja wa bima waliopata kadhia ya madai yake kukataliwa ni **Leo Logistics Co Ltd** ya **Dar es Salaam** ambaye madai yake yalikataliwa na UAP baada ya HANS kutopeleka ada za bima.

ii. **Kampuni ya Udalali wa Bima ya ENDEAVOUR.**

Kwa kampuni hii, moja ya wateja wa bima waliopata kadhia ya madai yao kukataliwa ni **Doreen Rutagumirwa** ambaye madai yake yalikataliwa na kampuni ya bima ya UAP kwa sababu Endevour Insurance Brokers hawakupeleka ada za bima.

iii. **Kampuni ya Udalali wa Bima ya LEGEND OF EAST AFRICA.**

Kwa kampuni hii, moja ya wateja wa bima waliopata kadhia ya madai yao kukataliwa ni **Benson Katanga** ambaye madai yake yalikataliwa na kampuni ya bima ya MGen kwa sababu hawakupeleka ada za bima yake hazikuwasilishwa.

iv. **Kampuni ya Udalali wa Bima ya SWIFT**

Pamoja na kosa la kutowasilisha ada za bima kwa makampuni ya bima, wamiliki wa kampuni wamefunga ofisi

bila kulipa ada stahiki na kufuata taratibu zilizowekwa za kufunga ofisi.

Ndugu waandishi wa Habari.

Aidha, pamoja na kufuta leseni za makampuni hayo hapo juu, Mamlaka inaendelea kushirikiana na **Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai** ili kuhakikisha wamiliki wa makampuni yafuatayo wanapatikana na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kuvunja Sheria ya Bima Na.10 ya mwaka 2009, kwani pamoja na kutowasilisha ada za bima kwa makampuni ya bima husika baada ya kupokea ada hizo kutoka kwa wateja, makampuni haya yamekuwa yakikwepa ukaguzi wa mara kwa mara wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na kutokufungua ofisi zao.

i. **Kampuni ya Udalali wa Bima ya PACIFIC**

Mmoja wa wateja waliopata adha ya kutofidiwa ni **Ndg. Rafai Mkumba** wa Dar es Salaam ambaye madai yake ya fidia yalikataliwa na kamapuni ya MGen baada ya kampuni ya udalali ya Pacific kushindwa kuwasilisha ada za bima.

ii. **Kampuni ya Udalali wa Bima ya CORE**

Mmoja ya wateja aliyeathirika na kitendo hiki cha kutokupeleka ada za bima ni **BQ Contractors Ltd** ya **Dar es**

Salaam ambaye madai yake yalikataliwa na UAP baada ya Core Insurance kutopeleka ada za bima.

Ndugu waandishi wa Habari na Wananchi.

Mamlaka imetathmini mwenendo wa makampuni haya na kuona ni vema ikachukua hatua za haraka zilizo ndani ya uwezo wake kwa mjibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya mwaka 2009 Kifungu cha 74, ambayo ni **kuyafutia leseni ya biashara** makampuni haya. Pia, ili kuhakikisha haki za wateja wa bima na heshima ya soko la bima inalindwa hata baada ya kampuni hizi kufutiwa leseni, Mamlaka imewasilisha taarifa zao kwa **Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (Director of Criminal Investigations - DCI)**. Hatua hizi madhubuti zimechukuliwa ili kuwalinda wateja, wafanyabiashara waadilifu wa bima na taifa kwa ujumla.

Ndugu waandishi wa Habari na Wananchi.

i. Niwaombe wananchi kutambua uwepo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini. Wananchi wasilalamike na kunung'unika pale wanapopata matatizo ya kibima kwa kutokujua wapi pa kwenda. Mamlaka, kupitia ofisi zetu za makao makuu na katika kanda zifuatazo: Nyanda za juu kusini (Mbeya; Jengo la NHC-Mtaa wa Lupa), Kanda ya Kati (Dodoma; jingo la LAPF-Mtaa wa Makole), Kanda ya Ziwa (Mwanza; Jengo la PPF

barabara ya Kenyatta), Kanda ya Kaskazini (Arusha; jingo la NSSF-Mtaa wa Kaloleni), Kanda ya Pwani (Dar es Salaam) na Ofisi ya Mamlaki visiwani (Zanzibar; Jengo la TIRA Mtaa wa Kilimani). iko tayari kusikiliza kila mwananchi, kikundi au taasisi iliyoonewa na makampuni ya bima tuliyosajili. Mamlaka iko imara katika kuhakikisha sekta za bima nchini inakuwa sehemu za chachu ya maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Dkt. Baghayo A. Saqware.

Kamishna wa Bima.